**Mwongozo wa kusahihisha.**

**1**.Hii ni kumbukumbu.Mtahiniwa azingatie vipengele viwili vya kissing vya kimsingi vya utungo wa aina hii.Muundo/sura na maudhui.

a) **SURA/MUUNDO**

Kichwa kikuu.Kijumuishe.

i)Jina la mkutano/kundi linalokutana

ii)Mahali pa mkutano

iii)Siku yabmkutano

iv)Tarehe ya mkutano

v) Saa

**b) Mahudhurio**

i)Waliohudhuria

ii)Waliotuma udhuru

iii)Waliokosa kuhudhuria

iv)waalikwa

**c)Ajenda**

**i)**kufunguliwa kwa mkutano

ii)Kusoma na kuthibitisha kwa kumbukumbu za mkutano wa awali.

iii)maswala ibuka.

iv) Ajenda kuu

- ✓ Umaskini kusababisha wizi
- ✓ Dawa za kulevya
- ✓ Marafiki wabaya
- ✓ Malezi mabaya
- ✓ Malezi mabaya k.m. mtoto akiiba na kupelekea wazazi, wazazi hawamuulizi alikotoa vitu hivyo.
- ✓ Tamaa ya mali kufanya watu kuiba, kushiriki ufisadi, n.k.
- ✓ Hasira au kushindwa kujidhibiti kusababisha kumpiga na kumuumiza mtu hata kumuua
- ✓ Chuki na wivu huweza kusababisha mauaji

v) Maswala mengineyo
vi) Kufunguliwa kwa mkutano

**2 a)** Ni insha ya hotuba. Izingatie mambo yafuatayo;

**a) Anwani**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- Anwani iwe fafanuzi. Itaje yafuatayo;
- Ni hotuba ya nani
- Ilitolewa wapi
- Inahusu nini
- Iandikwe kwa herufi kubwa
- Neno hotuba lazima litumiwe

**b) Utangulizi**

Utangulizi unaweza kuhusu mambo atakayoyashughulikia katika hotuba nzima.

Utangulizi ujitokeze katika aya ya kwanza.

**c) Mwili**

**Hoja nane zifuatazo zijadiliwe;**

- ✓ Kula chakula chenye virutubisho vyote na madini
- ✓ Kutotumia chumvi, sukari au mafuta mengi
- ✓ Kufanya mazoezi
- ✓ Kupimwa mara kwa mara
- ✓ Kupika vyakula vizuri
- ✓ Kunawa mikono na macho
- ✓ Kuchemsha maji au kuyatia dawa kabla ya kuyanywa
- ✓ Kutozini au kutumia kinga
- ✓ Chanjo kwa watoto
- ✓ Kutochangia vifaa kama vitana na nyembe na mavazi ili kujikinga na magonjwa ya ngozi.
- ✓ Kulala ndani ya neti iliyotiwa dawa
- ✓ Kufyeka nyasi karibu na nyumba na kutupa mikebe iliyo na maji
- ✓ Kuweka dawa kwenye vidimbwi ili kuua mbu
- ✓ Kutotumia vileo kama vile pombe na sigara
- ✓ Kuzuia kunyeshewa na mvua na kuvaa mavazi mazito wakati wa baridi au usiku
- ✓ Kukohoa au kupiga chafya mtu akiwa ameziba pua na midomo
- ✓ kutotema kikohozi ovyo.
- ✓ Kutubu dhambi, kujua Mungu na kuomba kwa afya ya kiroho.

**d) Hitimisho**

Atoe mhutasari wa hoja kuu alizozishughulikia.

Hutotea katika aya ya mwisho.

**b)** Hii ni insha ya methali:

**Maana ya methali:**mtu asipotia bidi katika jambo matiokeo yake huwa hafifu. Au kiasi cha kufanikiwa katika jambo hutegemea matayarisho au mikakati ambayo inawekwa.

Kisa kizingatie hali zifuatazio;


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ Mwanafunzi ambaye hatii bidii masomoni inavyostahili, hatilii kazi maanani na kila anapoelekezwa anapuuza. Wemzake wanatilia maanani kazi zao lakini yeye hufanya kidogo tu, baadaye anapata alama duni.
- ✓ Mlezi/mzazi kutowaelekeza na Watoto kuishia kuwa wa kutotegemewa.
- ✓ Mkulima akose kujiandaa ipatsavyo, hatimaye apate mavuno duni n.k

**c)** Hii ni insha ya mdokezo wa kumalizia.

Kisa kirejelee yafuatayo;

Mja ambaye amefanya uovu na hatishiki na uovu huo. Yaani anahalalisha maovu bila kujali.

**VIWANGO VYA INSHA.**

**KIWANGO CHA D (MAKI 01-05)**

Insha ya aina hii haieleweki.

Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia lugha na lugha yake ni hafifu hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika

Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa

Lugha imevurugika, uakifishaji haufai na insha ina makosa ya kila aina kisarufi kimaendelezo, kimtindo .

**KIWANGO CHA C (06 - 10)**

Mada haijakuzwa na kuendelezwa

Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia

Hana ubunifu wa kutosha

Huakifisha sentensi vibaya

Hana msamiati wa kuvutia wala msamiati mwafaka

Kuna makosa mengi ya sarufi, msamiati na hijai

**KIWANGO CHA B (11 – 15)**

Mtahiniwa anaonyesha kumudu lugha vilivyo
Mtahiniwa anadhirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza
Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri mfano sentensi ya neno moja, fupi na za mseto.
Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha
Mada huwa imekuzwa na kuendelezwa vikamilifu


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**KIWANGO CHA A (16-20)**

i Insha hii imezingatia urefu unaotakikana

ii Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mkato

- Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka
- Ana uwezo wa kutumia tamathali za lugha ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi
- Uumbaji wake unadhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri
- Kazi ya mtahiniwa ni nadhifu na hati ni nzuri.

UDHAIFU / MAKOSA KATIKA INSHA (YANAYOSHUSHA VIWANGO VYA ALAMA)

1. makosa ya sarufi
2. makosa ya hijai
3. maudhui
4. urefu
5. msamiati
6. sura / muundo
7. mtindo

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes